

TAARIFA FUPI YA MRADI WA VIKUNDI VYA VIJANA NA WANAWAKE WA JASIRIAMALI KWA NDUGU AMOUR HAMAD AMOUR KIONGOZI WA MBIO ZA MWENGE WA UHURU KITAIFA 2017

1.0. UTANGULIZI

Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa,

Wilaya ya Nkasi ina jumla ya vikundi **570**, vinavyofanya shughuli mbalimbali za ujasiriamali na kijamii. Kati ya vikundi hivi **260** ni vikundi vya wanawake, **220** ni vikundi mchanganyiko ME na KE na **90** ni vikundi vya vijana.

2.0. MADHUMUNI YA MRADI

Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa,

Lengo la uwepo wa vikundi vya vijana na wanawake ni kuboresha na kuimarisha hali ya maisha kiuchumi kwa vijana, wanawake na jamii. Aidha vikundi vinasaidia wanawake na vijana kujitegemea kiuchumi na kujiajiri na kuondoa dhana ya kutegemea ajira kutoka serikalini.

3.0. MANUFAA YA MRADI

Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa,

Mbele yako kuna jumla ya vikundi 7 vitakavyonufaika kupewa mikopo kwa ajiri ya kuendeleza miradi yao, vikundi vina jumla ya wanufaika 108 Me 44 na Ke 64. Vikundi hivyo ni: SKAUTI NAMANYERE wameshakabidhiwa mizinga **20** na kutundikwa eneo la Mfili yenye thamani ya Tshs. **3,000,000.00** vilevile vikundi vitatu (3) vya bodaboda vimeshakabidhiwa bodaboda **3** zenye thamani ya Tshs **6,000,000.00**.

Eneo hili la Uwanja wa Mkesha utakabidhi hundi yenye thamani ya Tshs. **2,000,000.00** kwa NKASI BEACH COOPERATIVE SOCIETY LTD, UPENDO USHIRIKA WAUZA SAMAKI na DAGAA watacabidhiwa hundi yenye thamani ya Tshs. **2,000,000.00** na KORONGWE SACCOS watacabidhiwa hundi yenye thamani ya Tshs **2,000,000.00** hivyo kufanya jumla ya Tshs. **15,000,000.00** kukopeshwa kwa mwaka wa fedha **2016/2017** huu ukiwa mchango kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi ikiwa ni utekelezaji wa agizo la serikali la kila Halmashauri kutenga **10%** kwa ajili ya kuwezesha makundi ya vijana na wanawake kujiinua kiuchumi.

4.0. HITIMISHO

Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa,

Tunamshukuru Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Joseph Pombe Magufuli kwa jitihada zake kushiriki kukuza urchumi wa viwanda kwa maendeleo ya nchi yetu.

Kwa heshima na taadhima sasa naomba ukabidhi fedha taslimu Tshs. **6,000,000.00** kwa vikundi vya wanawake na vijana vitatu (3).



**“SHIRIKI KUKUZA UCHUMI WA VIWANDA KWA MAENDELEO YA
NCHI YETU”**

Mwenge wa Uhuru 2017 Oyeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeee!

CLEOPHAS NKOSWE

KNY. MKURUGENZI MTENDAJI (W)

NKASI

TAARIFA FUPI YA UKAGUZI WA HIFADHI YA MSITU WA ASILI NA CHANZO CHA MAJI CHA MFILI KWA NDUGU AMOUR HAMAD AMOUR KIONGOZI WA MBIO ZA MWENGE WA UHURU KITAIFA 2017

1.0. UTANGULIZI

Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa

Hifadhi ya msitu na chanzo cha maji Mfili ilianzishwa mwaka 1998 chini ya sheria ndogo za Halmashauri za hifadhi ya mazingira na Vyanzo vya Maji ya mwaka 1998. Hifadhi ya msitu wa Mfili ina ukubwa upatao hekta **2,574.74** na hifadhi ya chanzo cha maji ina ukubwa wa hekta **347.13**. Ili kuhakikisha hifadhi hii inabaki salama mipaka yake imepimwa na kuwekwa alama za kudumu yaani mawe ya mipaka (bikoni). Jumla ya mawe ya mipaka nane (8) yenye wastani wa kimo cha sentimeta **100** na upana wa sentimeta **45** yamewekwa kwenye mipaka ya hifadhi. Aidha ukaguzi wa mara kwa mara umekuwa ukifanyika sambamba na kutoa elimu ya uhifadhi mazingira kwajamii ili kuhakikisha hakuna shughuli zozote za uharibifu wa mazingira zinazofanyika ndani ya hifadhi ya Msitu na chanzo cha maji Mfili.

2.0. GHARAMA ZA MRADI

Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa

Gharama za mradi ni Tshs. **14,413,000.00** kwa mchanganuo ufuatao:- Gharama za kupima na kuweka alama za kudumu za mipaka ambazo ni Tshs. **3,133,000.00**, gharama za ukaguzi kwa mwezi ni Tshs. **940,000.00** sawa na Tshs. **11,280,000.00** kwa mwaka.

3.0. MANUFAA YA MRADI

Ndugu kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa

Hifadhi ya msitu huu imewezesha kuendelea kuwepo kwa chanzo cha maji kilichopo ndani yake ambacho ni tegemeo kubwa kwa wakazi wa mji wa Namanyere. Hifadhi ya msitu huu itassaidia kwa kiwango kikubwa kupunguza majanga yatokanayo na mabadiliko ya tabia nchi ambayo yanababishwa na uharibifu wa mazingira kwa kukata miti ovyo. Majanga kama kuezuliwa kwa nyumba kutokana na upopo mkali na kimbunga, njaa kutokana na ukosefu wa mvua za uhakika yatapungua kwa kiasi kikubwa. Katika kuishirikisha jamii kuhifadhi mazingira, vikundi vya vijana vimewezeshwa kufanya shughuli za ufugaji nyuki kwa njia za kisasa katika hifadhi hii ambayo ni rafiki katika kutunza, kuhifadhi na kulinda msitu na chanzo cha maji. Msitu huu pia utatumwiwa na kikundi cha SKAUTI NAMANYERE kutundika mizinga **20** ambayo tayari umeikabidhi kwao kama ishara ya uendelevu katika utunzaji na ulinzi wa mazingira yetu.

4.0 HITIMISHO

Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa

Kwa heshima na taadhima tunaomba sasa ukague hifadhi ya msitu wa asili na chanzo cha maji cha Mfili.



**“SHIRIKI KUKUZA UCHUMI WA VIWANDA KWA MAENDELEO YA
NCHI YETU”**

Mwenge wa Uhuru 2017 Oyeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeee!

PASIAN ASENGA
K.N.Y. MKURUGENZI MTENDAJI (W)
NKASI

TAARIFA FUPI YA UZINDUZI WA MWALO WA SAMAKI KIRANDO KWA NDUGU AMOUR HAMAD AMOUR KIONGOZI WA MBIO ZA MWENGE WA UHURU KITAIFA 2017

1.0 UTANGULIZI

Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa

Mradi huu wa ujenzi wa mwalo wa samaki upo katika kijiji cha Mtakuja, Kata ya Kirando, Tarafa ya Kirando. Mradi ulijengwa kwa ufadhilli kutoka Mradi wa Hifadhi ya Bonde la ziwa Tanganyika (PRODAP). Mradi huu ulianza kujengwa katika mwaka wa fedha 2012/ 2013 baada ya kupata fedha hizo kutoka kwa wafadhilli na Mkandarasi SAXON BUILDING CONTRACTORS WA S. L. P 22347 DAR ES SALAAM alipewa tenda ya ujenzi wa mradi huu.

2.0 THAMANI YA MRADI

Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa

Mradi huu umetekeliza katika awamu mbili hadi kukamilika. Kiasi cha Tsh **653,485,584.00** katika awamu ya kwanza kilitolewa na PRODAP kujenga banda la soko, ghati, chanja, stoo, banda la kufungashia, uzio na choo. Awamu ya pili MIVARF walifadhili mradi na kutoa Tsh **357,807,500.00** ilikujenga chumba cha baridi (cold room) na kufanya mradi kugharimu jumla ya Tsh **1,011,293,084.00**.

3.0 MANUFAA YA MRADI

Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa

Mradi huu utawasaidia wavuvi wapatao **2,679** kutoka kata za Korongwe, Kirando, Kipili, Itete na Ninde kwa kuza samaki katika eneo moja kwalengo la kujiongezea kipato na pia kuisaidia Halmashauri kukusanya mapato yake kupitia ushuru wa samaki na dagaa, na ushuru washughuli zitakazofanyika eneo la soko.

Wastani wa tani **1,383** za samaki aina ya Migebuka, Kuhe, Sangara, Singa, Perege na tani **365** za dagaa zinatarajiwa kuuzwa katika soko hili kwa mwaka. Soko la samaki wabichi na wakavu ndani ya nchi hupatikana Wilaya ya Nkasi, Manispaa ya Sumbawanga na Jiji la Mbeya. Pia samaki wakavu kutoka katika soko hili wanatarajiwa kuuzwa nchi za Jamhuri ya Kidemokrasia Congo, Rwanda na Burundi.

3.0 HITIMISHO

Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa

Kwa heshima na taadhima tunaomba sasa uzindue mwalo wa samaki Kirando.



**“SHIRIKI KUKUZA UCHUMI WA VIWANDA KWA MAENDELEO YA
NCHI YETU”**

Mwenge wa Uhuru 2017 Oyeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeee!

REUBEN KAPONGO
KNY. MKURUGENZI MTENDAJI (W)

NKASI

TAARIFA FUPI YA HIFADHI YA MAZINGIRA SHULE YA SEKONDARI NKOMOLO KWA NDUGU AMOUR HAMAD AMOUR KIONGOZI WA MBIO ZA MWENGE WA UHURU KITAIFA 2017

1.0. UTANGULIZI

Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa

Mradi huu wa upandaji miti umeanzishwa mwaka 2016 katika shule za sekondari na shule za msingi ambapo miti ya aina mbalimbali imepandwa. Mradi huu ni sehemu ya utekelezaji wa maagizo ya serikali kwamba kila mwaka halmashauri ipande miti **1,500,000**. Halmashauri imezielekeza shule zote za msingi na Sekondari kuhakikisha kuwa zinapanda miti katika maeneo yao ambapo hadi sasa shule za Msingi **37** na Sekondari **18** zimekwishapanda miti ipatayo **21,270** ya aina mbalimbali. Hadi kufikia tarehe **30, April 2017** tunatarajia shule zote za msingi **104** na sekondari **23** zitakuwa zimepanda idadi ya miti ipatayo **74,019**.

Sambamba na shule zingine shule ya Sekondari Nkomolo ina jumla ya walimu **20**, Me ni **14** na Ke ni **6**, vilevile shule ina jumla ya wanafunzi **448**, Me ni **219** na Ke **229**, shule imepanda jumla ya miti **2,805** na iliyopo hai hadi sasa ni miti **2,500**. Kila mwanafunzi amepanda miti **4-5** na ataitunza hadi atakapohitim masomo ya kidato cha nne pia kila mwalimu amepanda mti mmoja na atautunza hadi atakapoondoka katika shule hii. Matarajio ya shule ni kuhakikisha mradi huu unakuwa endelevu.

3.0. GHARAMA ZA MRADI NA USIMAMIZI

Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa

Mradi huu unasimamiwa na uongozi wa shule na klabu ya mazingira ya wanafunzi. Mradi huu umegharimu Tshs. **1,925,000/=** pamoja na nguvu ya wanafunzi.

4.0. MANUFAA YA MRADI

Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa

Mradi huu utawezesha kupunguza majanga yatokanayo na mabadiliko ya tabia nchi ambayo yanababishwa na uharibifu wa mazingira kwa kukata miti ovyo. Majanga kama kuezuliwa kwa nyumba kutokana na upepo mkali na vimbunga, njaa kutokana na ukosefu wa mvua za uhakika yatapungua kwa kiasi

kikubwa.Pia mradi huu utasaidia kupatikana kwa nishati shulenii, mbao na kufanya mazingira ya shule kuwa ya kuvutia.

5.0. HITIMISHO

Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa

Kwa heshima na taadhima tunaomba sasa ukague mradi wa upandaji miti katika shule ya Sekondari Nkomolo kwa kupanda mti mmoja wewe binafsi kama ishara ya uzinduzi wa mradi huu.

“SHIRIKI KUKUZA UCHUMI WA VIWANDA KWA MAENDELEO YA NCHI YETU”

Mwenge wa Uhuru 2017 Oyeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeee!

PASIAN ASENGA
K.N.Y. MKURUGENZI MTENDAJI (W)
NKASI

**TAARIFA FUPI YA MRADI WA UJENZI WA MADARASA 2 NA OFISI
SHULE YA MSINGI LYAZUMBI KWA NDUGU AMOUR HAMAD AMOUR
KIONGOZI WA MBIO ZA MWENGE WA UHURU KITAIFA MWAKA 2017**

1. UTANGULIZI:

Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa,

Halmashasuri ya Wilaya ya Nkasi ina shule za Msingi **103** za Serikali na Shule ya binafsi 1. Kijiji cha Lyazumbi kipo kata ya Paramawe kina kaya **420** kipo umbali wa Km **6** kutoka Makao Makuu ya Kata.

2. MADHUMUNI YA MRADI

Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa,

Madhumuni ya kujenga shule hii ya Lyazumbi ni kutokana na idadi kubwa ya wanafunzi waliopo kijiji na umbali Km **6** kutoka kijiji cha Lyazumbi hadi shule ya msingi Paramawe. Wazazi waliomba kujenga shule ili kukabiliana na changamoto ya umbali huo. Hivyo shule ilianza kujengwa **Agosti 2016**, ambapo itakapokamilika wanafunzi wapatao **229** wataanza masomo, kati ya hao **106** ni darasa la awali, **91** darasa la I na **32** ni darasa la II.

3. GHARAMA ZA MRADI:

Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa,

Ujenzi wa vyumba **2** vya madarasa ni mionganini mwa vyumba vingine **273** vinavyoendelea kujengwa katika Wilaya ya Nkasi.

Mradi huu wa ujenzi wa vyumba 2 vya madarasa na Ofisi itakuwa na thamani ya Tsh. **38,950,000.00** hadi kukamilika kwake kwa mchanganuo ufuatao:-

- | | |
|----------------------|---------------------------|
| 1. Nguvu za Wananchi | Tsh. 28,590,000.00 |
| 2. Halmashauri | <u>Tsh. 10,360,000.00</u> |
| Jumla | Tsh. 38,950,000.00 |

Mradi huu wa ujenzi wa vyumba vya madarasa na ofisi unawakilisha ujenzi wa vyumba vya madarasa **48** vinavyoendelea kujengwa katika Wilaya ya Nkasi vilivyofikia usawa wa renta, ambapo hadi kukamilika vitakuwa na thamani ya Tsh. **960,000,000.00**. Vyumba vyote vikamilika vitakuwa na thamani ya Tshs. **6,420,000,000.00** ikiwa ni wastani wa chumba kimoja kugharimu sh. **20,000,000.00**

4. HITIMISHO:

Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa,

Tunaipongeza Serikali ya awamu ya **5** kwa kuimarisha sera ya Elimu bure katika Wilaya yetu.

Kwa heshima na taadhima tunakuomba sasa utuwekee jiwe la msingi.



**“SHIRIKI KUKUZA UCHUMI WA VIWANDA KWA MAENDELEO
YA NCHI YETU”**

Mwenge wa Uhuru Mwaka 2017 Oyeeeeeeeeeeeeeee

MISSANA KWANGURA
K.N.Y. MKURUGENZI MTENDAJI (W)
NKASI

TAARIFA FUPI YA UZINDUZI WA MADARASA SITA NA MATUNDU MANNE YA VYOO KWA NDUGU AMOUR KIONGOZI WA MBIO ZA MWENGE WA UHURU KITAIFA 2017

1.0. UTANGULIZI

Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa

Shule ya Sekondari Kirando ilianzishwa mwaka 2009, ina jumla ya walimu 17 na upungufu ni walimu 20 na ina jumla ya wanafunzi 758. Kabla ya mradi huu Kulikuwa na madarasa 10 na upungufu ulikuwa madarasa 11, vyumba hivyo vilikuwa havitoshelezi kulingana na idadi kubwa ya wanafunzi .

2.0. GHARAMA ZA MRADI

Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa

Mwezi Agosti 2016 Shule ilipokea fedha **Tsh 135,500,000.00** za ujenzi wa miundombinu ambao ulifanywa kupitia mafundi wa kawaida wanaoitwa **Madwallah** (local fundi) kwa gharama stahili, ujenzi uliana rasmi tarehe 11/ 11/ 2016 na kukamilika tarehe 16/ 02/ 2017 katika kipindi cha miezi mitatu kwa mgawanyo wa mafungu matatu kama ifuatavyo:

1. Ujenzi wa vyumba sita vya madarasa pamoja na dawati 240 Tsh **120,000,000.00**
2. Ujenzi wa vyoo matundu manne na chumba maalumu cha kubadilishia nguo wasichana **Tsh 5,500,000.00**
3. Ukarabati wa ofisi **Tsh 10,000,000.00**

3.0. MANUFAA YA MRADI

Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa

- Mradi umepunguza uhaba wa vyumba vya madarasa uliokuwepo kutoka vyumba 11 hadi 5.
- Mradi umeongeza idadi ya matundu ya vyoo vya wasichana kutoka vyoo 6 hadi 10.
- Mradi umeboresha jengo la utawala kwa kupanua ofisi ya walimu na mkuu wa shule.
- Mradi umewezesha kujengwa kwa chumba maalum cha wasichana.

4.0. HITIMISHO

Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa

Tunapenda kutoa shukurani za dhati kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania **Mh. Dr. JOHN POMBE MAGUFULI** kwa juhudini kubwa katika kutekeleza mipango yake thabiti ya kuweka mazingira mazuri ya kufundishia na kujifunzia kwa kupunguza uhaba mkubwa wa vyumba vyaa madarasa, uchakavu wa ofisi za walimu pamoja na upungufu wa matundu ya vyoo uliokuwa unaikabili shule hii.

Ndugu Miongozi wa Mbio za Mwenge Kitaifa kwa heshima na taadhima tunaomba sasa uzindue mradi huu.



**“SHIRIKI KUKUZA UCHUMI WA VIWANDA KWA MAENDELEO YA
NCHI YETU”**

“Mwenge wa Uhuru 2017 Oyyyyyyyyyyyyyyyyyyyy”

FORTUNATUS KAGUO
K.N.Y. MKURUGENZI MTENDAJI (W)
NKASI

TAARIFA FUPI YA UKAGUZI WA UFUGAJI BORA WA NG'OMBE KWA NDUGU AMOUR HAMAD AMOUR KIONGOZI WA MBIO ZA MWENGE WA UHURU KITAIFA 2017

1.0 UTANGULIZI

Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa

Wilaya ya Nkasi ina jumla ya ng'ombe **176,505** kati ya hao **5,508** ni ng'ombe bora wa nyama na **329** ni ng'ombe wa maziwa kwa mujibu wa sensa ya mifugo ya Wilaya ya 2016.

2.0 THAMANI YA MRADI

Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa

Mbele yako ni ng'ombe 44 bora wa nyama wanaomilikiwa na Ndugu Nyanda Kisinja wenyewe thamani ya Tsh **120,000,000.00**. Mfugaji huyu ni miogoni mwa wafugaji **5,884** Wilayani na ana jumla ya ng'ombe **460** wa kisasa ambao ni aina ya **Boran, Simental, Santa Getrudis na chotara wa ng'ombe** hao. Mfugaji huyu pia anamiliki eneo lenye ukubwa wa ekari **2,500**. Aidha mfugaji huyu ameweza kuwa mfugaji bora kwa kuzingatia kanuni na taratibu za ufugaji ikiwa ni pamoja na kuendeleza maeneo yake ya malisho, kuwapa ng'ombe chakula cha ziada mara watokapo malishoni, uogeshaji wa mifugo ili kuzuia magonjwa hassa ya kupe na kuweka kumbukumbu za mifugo yake.

3.0 MANUFAA YA MRADI

Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa

Mfugaji analenga kulifikia soko la juu la nyama nchini kwa kuzalisha ng'ombe bora kwakuwa ufugaji bora huongeza thamani ya mifugo na mazao yake hivyo kupelekeea kupata bei nzuri ya soko. Aidha kuitia mfugaji huyu atasaidia kutoa fursa kwa wafugaji wengine Wilayani kujifunza kwake ufugaji bora wa ng'ombe. Mfugaji pia amelenga kuanzisha kiwanda kidogo cha kuchakata maziwa yanayozalishwa shambani kwake ikiwa uzalishaji unafikia lita **26,400** kwa mwezi. Pia Halmashauri ya Wilaya inalenga kushirikiana na mfugaji kuona namna ya kuchakata kinyesi cha mifugo ili kupata gesi hivyo kupunguza uharibifu wa mazingira kwa kutumia nishati mbadala ya biogas pia Halmashauri inalenga kusaidia matengenezo ya miundombinu ya barabara kuingia na kutoka shambani kwake ambayo huwa haipitiki hasa wakati wa masika.

4.0 HITIMISHO

Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa

Kwa heshima na taadhima tunaomba sasa ukague ufugaji bora wa ng'ombe **44** wa ndugu Nyanda Kisinja.



**“SHIRIKI KUKUZA UCHUMI WA VIWANDA KWA MAENDELEO YA
NCHI YETU”**

Mwenge wa Uhuru 2017 Oyeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeee!

REUBEN KAPONGO
K.N.Y. MKURUGENZI MTENDAJI (W)
NKASI

TAARIFA FUPI YA MRADI WA NYUMBA BORA YA KULALA WAGENI KWA NDUGU AMOUR HAMAD AMOUR KIONGOZI WA MBIO ZA MWENGE WA UHURU KITAIFA 2017

1.0. UTANGULIZI

Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa

Mradi huu wa nyumba ya kulala wageni uliopo Kata ya Majengo ni moja kati ya nyumba za wageni zitakazoweza kutoa huduma bora ya malazi kwa wageni katika Wilaya ya Nkasi. Mradi huu ni endelevu kwani mwaka 2016 uliwekewa jiwe la msingi na Ndugu George Jackson Mbijima Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru 2016.

2.0. GHARAMA ZA MRADI.

Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa

Gharama za mradi huu ni kiasi cha Tshs. **250,000,000.00** ambapo nyumba hii inamilikiwa na Mhe. Desderius John Mipata Mbunge wa Jimbo la Nkasi Kusini.

3.0. MANUFAA YA MRADI

Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa

Kukamilika kwa mradi huu kutawezesha uboreshaji wa huduma za kulala wageni katika Wilaya yetu. Mradi huu unatarajia kunufaisha wananchi wa Kata ya Majengo kwa kupata ajira, vilevile kutoa huduma ya malazi kwa wageni ndani na nje ya Wilaya pamoja na Serikali kupata mapato.

4.0. HITIMISHO

Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa

Kwa heshima na taadhima sasa tunaomba uzindue nyumba hii ya kulala wageni.



**“SHIRIKI KUKUZA UCHUMI WA VIWANDA KWA MAENDELEO YA
NCHI YETU”**

Mwenge wa Uhuru 2017 oyeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeee!

CLEOPHAS NKOSWE

K.N.Y. MKURUGENZI MTENDAJI (W)

NKASI

TAARIFA FUPI YA KLABU YA WAPINGA RUSHWA NA KUPAMBANA NA DAWA ZA KULEVYA KWA NDUGU AMOUR HAMAD AMOUR KIONGOZI WA MBIO ZA MWENGE WA UHURU KITAIFA 2017

1.0. UTANGULIZI

Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa

Klabu ya Wapinga Rushwa na Dawa za Kulevya Shule ya Sekondari Nkomolo imeanzishwa mwaka 2017. Mlezi wa Klabu hii ni uongozi wa Shule ya Sekondari Nkomolo kwa kushirikina na TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA (TAKUKURU) na JESHI LA POLISI. Mpaka sasa Klabu hii ina jumla ya wanachama **130** kati yao wavulana ni **84** na wasichana ni **46**, Klabu nyingine zimefunguliwa katika shule zote za Sekondari zilizopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi.

2.0. THAMANI YA MRADI

Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa

Mradi wa uimarishaji wa Klabu ya Wapinga Rushwa na Dawa Kulevya umegharimu kiasi cha shilingi **289,000.00**

3.0. MADHUMUNI YA MRADI

Lengo la ufunguaji wa klabu hizi ni kuwajenga wanafunzi kimaadili na kuwashirikisha katika mapambano dhidi ya rushwa na dawa za kulevya kwa kufanya mambo yafuatayo:

1. Kuwezesha kutambua nafasi na wajibu wao katika mapambano dhidi ya rushwa na hivyo kushiriki ipasavyo kuzuia na kupambana na rushwa
2. Kuwajenga kimaadili kwa kuwafanya watambue madhara ya rushwa ili waichukie katika maisha yao na hatimaye kujenga jamii ya watu waadilifu.
3. Kuwezesha jamii kutambua nafasi na wajibu wao katika mapambano dhidi ya rushwa.
4. Kupinga matumizi ya dawa za kulevya na kutoa elimu juu ya athari ya dawa za kulevya.

Matarajio ya klabu hii ni kwamba wanafunzi ambao ni sehemu ya kundi la vijana ambao wanaaminika kama nguvu kazi ya Taifa katika Jamii, kupitia elimu ya athari za rushwa na matumizi ya dawa za kulevya wanatarajiwa kuwa

mabalozi wa kuelimisha vijana wenzao katika Jamii ya Nkasi na Tanzania kwa ujumla hata baada ya kuhitimu Masomo yao.

4.0. HITIMISHO

Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa

Kwa heshima na taadhima tunakuomba sasa uzindue Klabu ya Wapinga Rushwa na Dawa za Kulevyta katika shule ya Sekondari Nkomolo kama ishara ya uimarishaji wa Klabu hizo katika shule zote za Sekondari ndani ya Wilaya ya Nkasi.



**“SHIRIKI KUKUZA UCHUMI WA VIWANDA KWA MAENDELEO YA
NCHI YETU”**

Mwenge wa Uhuru 2017 Oyeeeeeeeeeeeeeeeeeee!

SAMSON M. BISHATI

KAMANDA WA TAKUKURU (W)

NKASI

TAARIFA FUPI YA SHUGHULI ZA VIWANDA VIDOGOVIDOGO KWA NDUGU AMOUR HAMAD AMOUR KIONGOZI WA MBIO ZA MWENGE WA UHURU KITAIFA 2017

1.0. UTANGULIZI

Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa,

Eneo hili ni eneo maalumu kwa shughuli za viwanda vidogovidogo lililotengwa na Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi, lenye ukubwa wa Square Meter za mraba **48,000** sawa na Hekta **4.8** Eneo hili lina viwanda vya, karakana za useremara; uchomeleaji, utengenezaji majiko banifu, usindikaji nafaka, mashine za kukoboa mpunga na mashine za kusaga mahindi.

2.0. GHARAMA ZA MRADI

Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa,

Gharama ya miradi iliyowekezwu katika eneo hili kwa sasa ina thamani ya Tshs. **98,000,000.00** ikijumuisha majengo, mashine na vitendea kazi. Vilevile Halmashauri ilihusika katika kutoa wataalamu wa kupima na kusimamia eneo hili la viwanda, kuhakikisha huduma ya umeme inapatikana eneo la viwanda na kutoa elimu ya uendeshaji biashara kwa ufanisi.

3.0. MADHUMUNI YA MRADI

Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa,

Madhumuni ya Mradi huu ni kutekeleza agizo la Serikali la kutenga maeneo maalumu kwaajili ya shughuli za vijana za uzalishaji mali, kilimo, michezo na kuwekewa miundombinu maalumu kama vile barabara, maji na umeme ili kuwawezesha kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi, kuwatambua na kuwawezesha kufanya kazi zenyet staha katika jamii. Vilevile katika kutambua mchango wa vijana katika kujitafutia ajira, Halmashauri imetoe pikipiki **3** ambapo kikundi cha BODABODA JIENDELEZE wanakabidhiwa pikipiki **1** zenyet thamani ya Tshs. **2,000,000.00**, kikundi cha BODABODA GROUP Namanyere watakabidhiwa pikipiki **1** zenyet thamani ya Tshs. **2,000,000.00**, kikundi cha BODABODA STENDI YA ZAMANI pikipiki **1** zenyet thamani ya Tshs. **2,000,000.00**.

Eneo hili pia kuna kikundi cha SKAUTI NAMANYERE ambao watakabidhiwa mizinga **20** zenyet uwezo wa kuzalisha wastani wa litu **400** na nta Kg **200** kwa

msimu mmoja ikiwa na thamani ya Tshs. **2,000,000.00** pia Tshs **1,000,000** zimetumika kwaajili ya ujenzi wa banda la kuweka mizinga katika msitu wa Asili wa mfilii. Kikundi kinatarajia kujipatia wastani wa Tshs **10,000,000.00** zitakazotokana na mauzo ya asali kwa mwaka.

4.0. HITIMISHO

Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa,

Tunamshukuru Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania **JOSEPH POMBE MAGUFULI** kwa jitihada zake katika kushiriki na kuhimiza dhana ya kukuza uchumi wa viwanda kwa maendeleo ya nchi yetu.

Kwa heshima na taadhima sasa tunakuomba ukague eneo hili la shughuli za viwanda vidogovidogo na kukabidhi fedha na pikipiki kwa vikundi.

**“SHIRIKI KUKUZA UCHUMI WA VIWANDA KWA MAENDELEO YA
NCHI YETU”**

Mwenge wa Uhuru 2017 Oyeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeee!

CLEOPHAS NKOSWE

K.N.Y. MKURUGENZI MTENDAJI (W)

NKASI

TAARIFA FUPI YA MRADI WA UJENZI WA ZAHANATI KWA NDUGU AMOUR HAMAD AMOUR KIONGOZI WA MBIO ZA MWENGE WA UHURU KITAIFA 2017

1.0 UTANGULIZI

Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa

Mradi huu wa ujenzi wa Zahanati katika Kijiji cha Mwai Kata ya Mtenga uliana mwaka 2014 Julai kwa nguvu za wananchi pamoja na Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi katika utekelezaji wa agizo la Serikali la kuwa na Zahanati katika kila kijiji Nchini.

2.0 GHARAMA ZA MRADI

Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa

Mpaka sasa mradi umegharimu jumla ya Tsh.**28, 960,000.00** Kwa mchanganuo ufuatao: Nguvu za wananchi sh. **18,960,000.00** na fedha kutoka Halmashauri Tsh. **10,000,000.00**. Mchanganuo wa fedha toka kwa wananchi ni kama ifuatavyo: mchanga Tsh. **1,150,000.00**, matofari Tsh. **7,500,000.00**, mawe Tsh. **1,050,000.00**, sementi Tsh. **4,620,000.00**, ndoo za maji Tsh **240,000.00**, ufundi Tsh.**3,700,000.00** na kokoto Tsh.**700,000.00**.

Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa

Mradi huu unakadiliwa kughalimu kiasi cha sh. **150,000,000.00** mpaka kukamilika kwake.

3.0 MANUFAA YA MRADI

Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa

Kukamilika kwa mradi huu kutasaidia kusogeza huduma za Afya kwa wakazi wa kijiji cha Mwai wapatao **3,666**. Huduma zitakazotolewa ni huduma za wagonjwa wa nje, huduma za uzazi na mtoto na huduma za chanjo.

Tunatoa pongezi za dhati kwa Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa jitihada zake zinazowezesha watoto wenyе umri chini ya miaka mitano, wazee wenyе umri wa kuanzia miaka sitini na zaidi na mama wajawazito kutibiwa bure.

4.0 HITIMISHO

Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa

Kwa heshima na taadhima sasa tunaomba utuwekee jiwe la msingi kwenye mradi huu wa Zahanati katika Kijiji cha Mwai.



“SHIRIKI KUKUZA UCHUMI WA VIWANDA KWA MAENDELEO YA NCHI YETU”

Mwenge wa Uhuru 2017 Oyeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeee!

DKT. EVERADA SANANE

K.N.Y. MKURUGENZI MTENDAJI (W)

NKASI

RAMANI YA WILAYA YA NKASI



**RATIBA NA MIRADI ITAKAYOPITIWA NA MBIO ZA MWENGE WA
UHURU 2017**

TAREHE	MAHALI	KM	MUDA	SHUGHULI/TUKIO	MHUSIKA
7/4/2017	Ofisi ya DC	00	12:00 – 01:00	Viongozi wa Nkasi kukusanyika	DC
	Ofisi ya DC	36	01:00 – 01:40	Kuondoka kuelekea Kizi	 OCD
	Kizi	00	01:40 - 03:00	<ul style="list-style-type: none"> • Mkuu wa Mkoa wa Katavi kumkabidhi Mwenge Mkuu wa Mkoa wa Rukwa • Mkuu wa Mkoa wa Rukwa kumkabidhi Mwenge Mkuu wa Wilaya ya Nkasi 	RC – Katavi RC – Rukwa DC – Nkasi
	Kizi	04	03:00 – 03:10	Kuondoka kuelekea Lyazumbi	 OCD
	Lyazumbi	00	03:10 – 03:25	Kuweka jiwe la msingi Madarasa 2 na ofisi 1	DC
	Lyazumbi	10	03:25 – 03:35	Kuondoka kuelekea Mwai	 OCD
	Mwai	00	03:35 – 04:00	<ul style="list-style-type: none"> • Kuweka jiwe la msingi jengo la Zahanati • Ujumbe wa Mwenge 	DC
	Mwai	10	04:00 – 04:15	Kuondoka kuelekea Mkole	 OCD
	Mkole	00	04:15 – 04:35	Ukaguzi wa ufugaji bora wa ngo'mbe	 DC
	Mkole	01	04:35 – 04:40	Kuondoka kuelekea sekondari ya Mkole	 OCD
	Sekondari ya Mkole	01	04:40 – 05:10	 CHAI	 DED
	Sekondari ya Mkole	13	05:10 – 05:20	Kuondoka kuelekea Isunta	 OCD
	Isunta	00	05:20 – 05:40	Uzinduzi wa nyumba ya mwananchi ya kulala wageni.	DC

	Isunta	03	05:40 – 05:45	Kuondoka kuelekea Nkomolo	OCD
	Nkomolo	00	05:45 – 06:10	<ul style="list-style-type: none"> • Ukaguzi wa shughuli za viwanda vidogo vidogo • Kukabidhi pikipiki 3 kwa Vikundi 3 vya Bodaboda • Kukabidhi mizinga 20 kwa kikundi cha Skauti 	DC
	Nkomolo	01	06:10 – 06:15	Kuondoka kuelekea sekondari ya Nkomolo.	OCD
	Sekondari ya Nkomolo	00	06:15 – 06:45	<ul style="list-style-type: none"> • Uzinduzi wa Klabu ya wapinga Rushwa na Dawa za kulevyia na ukaguzi wa hifadhi ya mazingira • Mkimbiza Mwenge Kitaifa kupanda mti • Ujumbe wa Mwenge 	DC
	Sekondari ya Nkomolo	00	06:45 – 07:15	CHAKULA CHA MCHANNA	DED
	Sekondari ya Nkomolo	05	07:15 – 07:20	Kuondoka kuelekea Mfilii	OCD
	Mfilii	00	07:20 – 07:35	<ul style="list-style-type: none"> • Ukaguzi wa hifadhi ya msitu wa asili na chanzo cha maji 	DC
	Mfilii	60	07:35 – 08:55	Kuondoka kuelekea Kirando	OCD
	Kirando	00	08:55 – 09:10	Uzinduzi wa Mwalo wa Samaki	DC
	Kirando	03	09:10 – 09:15	Kuondoka kuelekea sekondari ya Kirando	OCD
	Sekondari ya kirando	00	09:15 – 09:25	<ul style="list-style-type: none"> • Ufunguzi wa madarasa 6 na matundu 4 ya vyoo vya wasichana • Mkimbiza Mwenge Kitaifa Kuwashaa Umeme Shuleni 	DC

	Sekondari ya Kirando	00	09: 25– 09:30	Kuondoka kuelekea uwanja wa mkesha	OCD
	Uwanja wa mkesha	00	09:30 –09:50	<ul style="list-style-type: none"> • Ukaguzi wa shughuli za vikundi vya vijana na akina mama wajasili amali • Kukabidhi hundi kwa vikundi 3 vya SACCOS za vijana na wanawake 	DC
	Uwanja wa mkesha	00	09:50 – 10:05	Ukaguzi wa banda la uchangiaji damu, upimaji wa VVU, Malaria, na upimaji wa viashiria vya magonjwa yasiyoambukiza.	DC
	Uwanja wa mkesha	00	10:05 – 10:35	Kusoma Risala ya Utii kwa Mhe. Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania	DAS/ DED
	Uwanja wa mkesha	00	10:35 – 10:50	Kutambulisha wageni	DC
	Uwanja wa mkesha	00	10:50 – 10:55	Burudani	DC
	Uwanja wa mkesha	00	10:55 – 11:25	Ujumbe wa Mwenge	DC
	U/ mkesha	00	11:25 – 01:30	Burudani	DC
	Sekondari ya Kirando	00	01:30 – 02:30	CHAKULA CHA JIONI	DED
	U/ mkesha	00	02:30 – 10:30	Mkesha/ burudani	DC
	JUMLA YA KM	146			
8/4/2017	MAHALI	KM	MUDA	SHUGHULI/TUKIO	MHUSIKA
	Sekondari	00	10:30 -11:30	CHAI	DED

ya Kirando				
Uwanja wa mkesha	160	11:30 – 02:00	Kuondoka kuelekea Katuka	OCD
Katuka	00	02:00 – 02:30	Mkuu wa Wilaya ya Nkasi kumkabidhi Mwenge Mkuu wa Wilaya ya Kalambo	DC – Nkasi DC – Kalambo
JUMLA KUU YA KM	306			

THAMANI YA MIRADI YA MAENDELEO ITAKAYOTEMBELEWA NA MBIO ZA MWENGEWA UHURU 2017

NA	JINA LA MRADI	IDARA	MAHALI ULIPO	HATUA YA UTEKELEZAJI	GHARAMA ZA WACHANGIAJI				
					H/SHAURI	WAHISANI	WANANCHI	SERIKALI KUU	JUMLA KUU
1	Madarasa 2 na Ofisi 1	Elimu Msingi	Lyazumbi	Ujenzi Unaendelea	10,360,000.00	-	28,590,000.00	-	38,950,000.00
2	Ufugaji Bora wa Ngo'mbe	Mifugo	Mkole	Ufugaji Unaendelea	-	-	120,000,000.00	-	120,000,000.00
3	Jengo la Zahanati	Afyा	Mwai	Ujenzi Unaendelea	10,000,000.00	-	18,960,000.00	-	28,960,000.00
4	Nyumba ya Mwananchi ya Kulala Wageni	Maendeleo ya Jamii	Isunta	Imekamilika	-	-	250,000,000.00		250,000,000.00
5	Shughuli za Viwanda Vidogovidogo	Maendeleo ya Jamii	Nkomolo	Shughuli Zinaendelea	-	-	98,000,000.00	-	98,000,000.00
6	Hifadhi ya Mazingira	Maliasili	Nkomolo	Ipo Katika Hali Nzuri	1,425,000.00	-	500,000.00	-	1,925,000.00
7	Klabu ya Wapinga Rushwa na Dawaza Kulevya	Utawala	Nkomolo	Ipo Inaendelea	289,000.00	-	-	-	289,000.00
8	Hifadhi ya Msitu wa Asili na Chanzo cha Maji	Maliasili	Mfili	Ipo Katika Hali Nzuri	14,413,000.00	-	-	-	14,413,000.00
9	Madarasa 6 na Matundu 4 ya Vyoo vya Wasichana	Elimu Sekondari	Kirando	Yamekamilika	-	-	-	135,000,000.00	135,500,000.00
10	Mwalo wa Samaki	Mifugo/ Uvuvu	Kirando	Umekamilika	-	1,011,293,083.00	-	-	1,011,293,083.00
11	Vikundi vya Vijana na Wanawake Wajasiliamali	Maendeleo ya Jamii	Nkomolo na Kirando	Vipo Vinaendelea	15,000,000.00				15,000,000.00
	JUMLA KUU				51,487,000.00	1,011,293,083.00	516,050,000.00	135,000,000.00	1,714,330,083.00